



NOOR
International

Anajua yaliyo ndani yako



noor.gallery

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

● Kwa jina la Allah Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu ●

هَكَذَا نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ
فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَكِنَّ الظَّالِمِينَ
بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴿٣٣﴾

[الأَنْعَام: ٣٣]

Hakika, tunajua kuwa kwa yakini kabisa,
yanakuhuzunisha mno yale wanayosema.
Kwa hakika hawakupingi wewe, lakini
madhalimu wanazipinga Aya za Allah

Qurani (6:33)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



۞ لِيُنْفِقْ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ ۗ وَمَن قُدِرَ
 عَلَيْهِ رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ لَا
 يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَّا آتَاهَا سَيِّجَعُلُ اللَّهُ
 بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٧﴾
 [الطَّلَاق: ٧]

Ili mwenye wasaa agharimu kwa wasaa
 wake, na aliyebaniwa riziki yake, basi
 agharimie katika kile Alichompa Allah.
 Allah Hamkalifishi mtu yeyote yule
 isipokuwa kwa kile Alichompa. Allah
 Atajaalia baada ya ugumu kuwa wepesi

Qurani (65:7)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَنَعَلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِ نَفْسُهُ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾﴾

[ق: ١٦]

Na kwa yakini Tumemuumba Mtu na Tunajua yale inayowaza nafsi yake, na Sisi Tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake

Qurani (50:16)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



فَبَدَأَ بِأَوْعِيَّتِهِمْ قَبْلَ وِعَاءِ أَخِيهِ ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا مِنْ
وِعَاءِ أَخِيهِ كَذَلِكَ كِدْنَا لِيُوسُفَ مَا كَانَ لِيَأْخُذَ أَخَاهُ فِي
دِينِ الْمَلِكِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَن نَّشَاءُ
وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ ﴿٧٦﴾

[يوسف: ٧٦]

Basi (Yule mpekuzi) alianza kwenye mizigo yao kabla ya mzigo wa ndugu yake. Kisha alilitoa (bakuli lililoibwa) kutoka katika mzigo wa ndugu yake. Hivi ndivyo tulivyomfunza Yusuf mbinu (ya kubaki na nduguye). Asingeweza kumchukua ndugu yake kwa sharia ya mfalme isipokuwa kwa matakwa ya Allah. Tunawainua daraja nyingi tuwatakao na juu ya kila anayejua yupo anayejua zaidi

Qurani (12:76)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





NOOR
International

هُم مِّنْ أَهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِۦ وَمَنْ ضَلَّ
فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ وَمَا كُنَّا
مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾

[الإسراء: ١٥]

Anaye ongoka basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake. Na anaye potea basi anapotea kwa hasara yake mwenyewe. Wala habebi mbebaji mzigo wa mwengine. Wala Sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke Mtume

Qurani (17: 15)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



فَتَعَلَىٰ اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ وَلَا تَعْجَلْ
بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ
وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١١٤﴾

[طه: ١١٤]

*Ametukuka Allah, Mfalme wa Haki.
Wala usiifanyie haraka hii Qur'ani,
kabla haujamalizika ufunuo wake. Na
sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie
ilimu*

Qurani (20: 114)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



۞ الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ
 فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ
 الْوَكِيلُ ﴿١٧٣﴾ فَأَنْقَلَبُوا بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ لَّمْ يَمَسَّهُمُ
 سُوءٌ وَاتَّبَعُوا رِضْوَانًا مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ ﴿١٧٤﴾

[ال عمران: ١٧٣-١٧٤]

**Ambao watu waliwaambia wao: hakika kundi la
 watu limekukusanyikieni basi waogopeni, hilo
 likawazidishia imani na wakasema: Allah
 anatutosha na ndiye mbora wa wenye
 kutegemewa Basi wakarudi na neema za Allah na
 fadhila zake, hakuna baya lililowagusa, na
 wakafuata yanayomridhi Allah, na Allah ni
 mwenye fadhila kubwa mno**

Qurani (3: 173-174)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿قُلْ يَاعِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ﴾ ﴿٥٣﴾

[الزمر: ٥٣]

Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Allah. Hakika Allah husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu

Qurani (39: 53)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا

السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

[التوبة: ٤٠]

Ikiwa nyinyi hamtamnusuru Mtume (Muhammad), basi Allah alikwishamnusuru pale waliokufuru walipomtoa (walipomfukuza) akiwa mmoja kati ya wawili wakati walipokuwa kwenye pango (la mlima Thaur), wakati akimwambia Swahibawake: “Usihuzunike. Hakika, Allah yupo pamoja nasi”. Allah alimteremshia utulivu wake, na akampa nguvu kwa majeshi ambayo hamkuyaona, na akalifanya neno la waliokufuru kuwa chini sana, na Neno la Allah ndilo lililo juu zaidi. Na Allah ndiye Mwenye nguvu mno, Mwenye hekima sana

Qurani (9: 40)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



إِنَّا أَنشَأْنَاهُنَّ خِيَارًا لِّمَن يَتَّقَىٰ ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

[النحل: ١٢٨]

Kwa hakika Allah yupo pamoja na wale wanaomcha (Allah), na wale wafanyao wema

Qurani (16: 128)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA





NOOR
International

 noor.gallery